HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, MHESHIMIWA CELINA OMPESHI KOMBANI (MB) WAKATI AKIFUNGUA MKUTANO WA BARAZA KUU LA PILI LA WAFANYAKAZI KATIKA UTUMISHI WA UMMA – TANZANIA BARA, KATIKA HOTELI YA ST. GASPAR, DODOMA TAREHE 21 JUNI, 2012

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma,

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Wafanyakazi katika

Utumishi wa Umma,

Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma,

Ndugu Katibu wa Baraza Kuu la Wafanyakazi katika

Utumishi wa Umma,

Ndugu Wajumbe wa Baraza,

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Habarini za asubuhi,

Ndugu Mwenyekiti, Awali ya yote naomba nichukue fursa hii kuwashukuru kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika ufunguzi wa Mkutano huu wa Pili wa Baraza Kuu la Pili la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma – Tanzania Bara, ambao kwangu utakuwa ni wa kwanza kufuatia mabadiliko ya Baraza la Mawaziri yaliyotokea hivi karibuni. Napenda pia nichukue fursa hii kuwapa pole kwa safari, maana naelewa wengi mmetoka katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, na mmetumia muda mrefu njiani kuweza kufika kwenye kikao hiki ili kufanikisha malengo ya Baraza.

Nawashukuru sana

Ndugu Mwenyekiti, Naomba pia nichukue fursa hii kuupongeza kwa dhati uongozi wa Mkoa wa Dodoma nikianza na Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa, Mkurugenzi wa Halmashauri, na viongozi wa vyama vya wafanyakazi wa Mkoa wa Dodoma kwa ushirikiano waliotuonyesha na kutuwezesha kufanya mkutano huu hapa Dodoma. Vile vile namshukuru mwenyekiti wa Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma, Bw. George D. Yambesi na kuwapongeza wale wote waliohusika katika maandalizi ya Mkutano huu na shughuli nzima kwa ujumla.

Ndugu Mwenyekiti , Nitakuwa sina fadhila kama nitaacha kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Hawa A. Ghasia , ambaye amehamia Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, **TAMISEMI** kwa kazi nzuri aliyoifanya wakati akiwa Waziri mwenye dhamana ya Utumishi wa Umma, kwa kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unatimiza malengo yake kama inavyotakiwa. Nami nitajitahidi kuendeleza pale alipoachia na kuhakikisha kuwa Watumishi wa Umma wanashirikishwa kwa ukamilifu katika masuala yanayowahusu na hivyo kuweza kuongeza tija na hatimaye kuongeza ubora wa maisha ya watanzania kwa ujumla.

Ndugu Mwenyekiti, Nimeelezwa kuwa huu ni mkutano wenu wa pili toka mlipoteuliwa kuwa wajumbe wa Baraza hili la pili la Wafanyakazi Katika Utumishi wa Umma. Nimeelezwa pia kuwa katika kipindi hiki kifupi mmeweza kujadili na kupitisha mambo mbalimbali yanayohusu Watumishi ikiwa ni pamoja na kujadili na kupitisha miundo mbalimbali ya Watumishi. Aidha, katika kutekeleza majukumu yenu, suala la uundwaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi sehemu za kazi limeendelea kupewa kipaumbele na nimefurahi kusikia kuwa karibu maeneo yote ya kazi katika utumishi wa umma sasa yana Mabaraza ya wafanyakazi. **Nawapongeza sana.** Tuendelee kushirikiana kufuatilia ili kuhakikisha Mabaraza haya kweli yanakutana na kufanya kazi zake.

Ndugu Mwenyekiti, Tarehe 08/06/2012 nilikutana na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi vyenye Wanachama katika Utumishi wa Umma kwa madhumuni ya kufahamiana. Katika mazungumzo yetu, nilieleza nia yangu ya kuwa karibu na wafanyakazi ili kwa pamoja tuweze kujenga mazingira ya kuaminiana na hivyo kuleta ufanisi. Nafurahi kuwa wote kwa pamoja tulikubalina pia kutumia mifumo tuliyonayo ya Majadiliano, na pale inapobidi, tuweze kuiboresha zaidi mifumo hiyo. Japo muda ulikuwa mfupi, tulizungumzia baadhi ya Changamoto zinazoukabili Utumishi wa Umma na umuhimu wa kuendelea kuzishughulikia. Changamoto kubwa ninayoiona ni mishahara midogo isiyokidhi mahitaji, hali ambayo imesababisha migogoro mbalimbali ya kiutumishi. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa suala la mishahara linategemea pamoja na mambo mengine, ubora wa tija katika Taasisi zetu. Nafurahi kusikia kuwa katika Mkutano huu mtajadili Mada kuhusu Tija kwa kuwa sote tunaelewa kuwa bila tija hata maslahi mbalimbali ya Watumishi yatakuwa ni kitendawili. Ni mategemeo yangu kuwa mkutano huu na mingine itakayofuata mtajadili na kuona namna ya kuongeza tija ili mishahara na maslahi mbalimbali ya Watumishi yaweze kuongezeka.

Ndugu Mwenyekiti, *Pamoja* na kuongeza tija ni muhimu kutambua kuwa mahitaji ni mengi kuliko uwezo wa Serikali na ndio maana Serikali imekuwa ikiandaa Mipango na Programu za utekelezaji. Nimefurahi kuambiwa kuwa katika ajenda zenu wajumbe wataelimishwa na kujadili kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano pamoja na Mfumo wa Bajeti ya Serikali, ambayo nidyo nyenzo kubwa ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo. Ni matumaini yangu kuwa elimu itakayopatikana kupitia Mada hizi itawasidia kuwaelimisha Watumishi umuhimu wa kujua kuhusu vipaumbele vya Taifa kwa miaka mitano ijayo pamoja na mfumo mzima wa bajeti ya serikali. Watumishi wakipata uelewa kuhusu vipaumbele vya taifa wataweza kupata misingi ya kudai Maslahi badala ya sasa ambapo madai hayawiani na uwezo wa Serikali kuyatekeleza.

Ndugu Mwenyekiti , Pamoja na mipango ya Kitaifa, naelewa kuwa katika Utumishi wa Umma kuna jitihada nyingi zinazoendelea zilizobuniwa kukabiliana na changamoto zinazojitokeza mara kwa mara ikiwemo ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu za kazi. Programu za mabadiliko katika Utumishi wa Umma zilizobuniwa kwa ajili hiyo ni pamoja na Programu za mabadiliko katika Utumishi wa Umma, Serikali za Mitaa (LGRP), Sekta ya Fedha (PFRP), Sekta ya Sheria (LSRP) na Mkakati wa Kupunguza na Kupambana na Rushwa (NACSAP). Pamoja na programu hizi, ipo Mipango mingine yenye lengo la kuondoa kero za Watumishi hususan Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara ujulikanao kama "HCMIS". Mfumo huu siyo tu huenda umeondoa tatizo la Watumishi hewa, bali pia umeondoa tatizo la Watumishi wapya kuchelewa kulipwa mishahara. Aidha, mfumo huu utasaidia kuondoa kero kwa Wastaafu ambao wamekuwa wakisumbuliwa kupata mafao kutokana na kukosekana kumbukumbu muhimu.

Ndugu Mwenyekiti, Katika ajenda zenu nimeona kuwa mtajadili na kupitisha Miundo mbalimbali ya Maendeleo ya Watumishi. Napenda kusisitiza kuwa Miundo ya Maendeleo ya Watumishi ndiyo inayotoa maelekezo kuhusu sifa zinazohitajika kwa mtu yeyote kuweza kuajiriwa kazini na kupanda cheo katika Utumishi wa Umma. Napenda kusisitiza kuwa miundo hii iangaliwe kwa umakini ili kuona kama inatimiza malengo yaliyokusudiwa na kuwawezesha Watumishi wa Umma kuendelea kubakia katika Utumishi wa Umma.

Ndugu Mwenyekiti, Kabla ya kumaliza hotuba yangu, naomba nizungumzie Mwelekeo wa Serikali kuhusu namna bora ya kuwianisha Mishahara katika Utumishi wa Umma. Kama wote tunavyofahamu, Serikali ilipitisha Sera ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010. Sera hii, inatokana pamoja na mambo mengine, na Mapendekezo ya Tume ya Rais ya Kuboresha Mishahara ya Mwaka 2006 maarufu kama Tume ya Ntukamazina. Kwa sasa Serikali inakamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hii, kama njia ya utekelezaji wa Sera hiyo. Aidha, Serikali imeanzisha Bodi ya Mishahara na Maslahi, ambayo pamoja na mambo mengine, itakuwa na jukumu la kuwianisha (Rationalize) na kuoanisha (Harmonize) mishahara ya watumishi wote wanaopata mishahara kutoka HAZINA. Bodi itaanza kazi rasmi katika mwaka wa fedha wa 2012/2013. Nawaomba Wajumbe wa Baraza hili muipe ushirikiano Bodi ili tuweze kuondoa kasoro zilizopo katika Mfumo wetu wa Mishahara.

Ndugu Mwenyekiti , Baada ya kusema haya, naomba tena kuwashukuru kwa kunialika, na ni mategemeo yangu kuwa mtatumia nafasi yenu ya kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali, ili Serikali iweze kuondokana na kero mbalimbali za Watumishi, na hivyo kuleta ufanisi katika mifumo yetu, kujenga motisha na ari ya kazi ili tuendelee kutoa huduma bora na zenye viwango kwa wananchi.

Baada ya kusema haya, naomba sasa nitamke kuwa mkutano huu wa Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma, umefunguliwa rasmi.

Asanteni kwa kunisikiliza